

MILAMBO CO - OPERATIVE UNION LIMITED

MILAMBO CU (2018) LTD - REG. NO AFF-TBR-URA-DC-2023-57

Telegraph: 'MILAMBO'
Tel:
Mob: 255765-567-584
Fax:
E-Mail:
milambocultd@gmail.com



Bomani Road,
P.O. Box 186,
URAMBO.

Kumb Na.AC7/7/199/01/39

04 MAY, 2026.

TANGAZO LA ZABUNI YA UFUNDI WA UWEKAJI MIFUMO YA UMEME, MAJI SAFI NA TAKA.

1.0 UTANGULIZI

Milambo Co-operative Union Limited (2018) Ltd ilianzishwa mwaka 2018 kufuatia kujitenga na Chama Kikuu cha Ushirika WETCU. Makao makuu ya chama yako katika Wilaya ya Urambo, na kinaendesha shughuli zake kwa mujibu wa **Sheria ya Vyama vya Ushirika Na. 6 ya mwaka 2013 (kama ilivyorekebishwa mwaka 2025)**. Chama kimesajiliwa rasmi kwa namba **AFF-TBR-URA-DC-2023-57**.

Katika kuendeleza mipango yake ya maendeleo na kuimarisha huduma kwa wanachama wake, **Milambo Co-operative Union Ltd (2018)** inaendelea kutekeleza **mradi wa ujenzi wa jengo la biashara (MILAMBO COMMERCIAL COMPLEX) na ukumbi wa mikutano** katika wilaya ya Kaliua, mkoa wa Tabora.

Utekelezaji wa mradi huu unaendelea kwa utaratibu wa **FORCE ACCOUNT**. Hivyo, wananchi wote wenye sifa, uzoefu na uwezo katika upande wa uwekaji wa mfumo wa umeme na mfumo wa maji safi na taka wanakaribishwa kutuma maombi yao ili kushiriki katika utekelezaji wa kazi za mradi huu.

2.0 SIFA ZA MUOMBAJI:

- i. Awe na uwezo wa kusoma ramani na kuitafsiri vizuri.
- ii. Awe na uzoefu wa kufanya kazi na taasisi za umma/majengo ya serikali.
- iii. Muombaji (fundi mkuu) wa mfumo wa umeme awe na elimu ya kuanzia daraja la pili na awe amesajiliwa na EWURA kwa kazi za umeme.
- iv. Muombaji (fundi mkuu) wa mfumo wa maji awe na elimu ya kuanzia daraja la pili kutoka katika chuo cha ufundi stadi veta au chuo chochote kinacho tambulika na serikali.

- v. Muombaji awe na uzoefu wa kufanya kazi na serikali au taasisi binafsi ndani ya miaka mitano kwa kazi za uwekaji wa mifumo ya umeme au uwekaji wa mifumo ya maji safi na taka kwa kuambatanisha nyaraka za maeneo aliyofanya kazi hizo kama Mikataba, Hati za Malipo n.k
- vi. Awe mwaminifu na mwadilifu.
- vii. Awe na mafundi wenye uzoefu katika maswala ya umeme, AC, CCTV camera.
- viii. Uwepo wa mtaalamu katika upande wa Teknolojia ya habari na mawasiliano (ICT) itakuwa sifa ya ziada kwa muombaji wa kazi ya uwekaji mfumo wa umeme.
- ix. Muombaji wa zabuni ya mfumo wa maji safi na taka awe na mafundi wenye uzoefu katika kazi hizo.
- x. Awe na mafundi wasaidizi wakutosha wenye uwezo mzuri na awe na uwezo wa kuwasimamia.
- xi. Awe na mtaji wa kuanzia kwani hakutakuwa na malipo ya awali bali atalipwa kulingana na gharama ya kazi itakayokuwa imefanyika na kukubaliwa na mhandisi wa ujenzi.
- xii. Awe na TIN namba na Akaunti Namba

3.0 MASHARTI YA KUTUMA MAOMBI:

- i. Muombaji anatakiwa kufika na kuona sehemu na mazingira ambapo kazi hizo zitafanyika.
- ii. Kabrasha za zabuni zinapatikana kwa njia ya kielektroniki kuanzia saa 2:00 asubuhi hadi saa 10:00 alasiri.
- iii. Muombaji aonyeshe gharama zake kwa kujaza kabrasha la zabuni na kurudisha likiwa limefungwa/kutuma kwa njia ya mtandao.
- iv. Mwisho wa kutuma maombi ni tarehe 11/05/2026 saa 5:00 Asubuhi na ufunguzi utafanyika mara baada ya kufunga zoezi hilo katika ofisi za Chama Kikuu cha Ushirika Milambo.
- v. Waombaji/wawakilishi wanaruhusiwa kuhudhuria ufunguzi huo.
- vi. Muombaji aonyeshe muda na mpango kazi atakaotumia kufanya na kukamilisha kazi hiyo.
- vii. Ada ya Maombi ni Shilingi **200,000/=** (laki mbili tu) kwa waombaji wa kazi ya uwekaji mfumo wa maji safi na taka na Shilingi **300,000/=**(laki tatu tu) za kitanzania kwa waombaji wa kazi ya uwekaji mfumo wa umeme ambayo itatolewa wakati wa kuchukua kablasha kama gharama za ununuzi na haitorudishwa.
- viii. Maombi yatumwe kwa njia ya kielektroniki kupitia E-mail milambocultd@gmail.com
Au kupitia anuani hapo chini;

Meneja Mkuu,

***Chama Kikuu cha Ushirika Milambo,
S.L.P 186, Urambo-Tabora.***

KAZI ZITAKAZOFANYIKA:

- *UWEKAJI WA MFUMO WA UMEME*
- *UWEKAJI WA MFUMO WA MAJI SAFI NA TAKA.*

NB:

- Maelezo ya kina ya kazi yanapatikana kupitia michoro na nyaraka za zabuni.
- Muombaji anaruhusiwa kuomba kazi zaidi ya moja kwa kuambatanisha nyaraka za uzoefu wa kila kazi aliyoomba
- Kwa mawasiliano zaidi tafadhali tupigie kupitia namba
+255 756 319 641 AU +255 717 523 644

Malipo yote yafanyike kupitia Akaunti za Benki

MILAMBO CU.LTD

NMB – 51310019476

CRDB – 0150374252600

“Pamoja na Salamu za Ushirika”

.....
Innocent J. Tibesigwa
MENEJA MKUU.

